

## MAANDALIZI YA SHAMBA LA MIZABIBU NA UPANDAJI

### Sifa za eneo linalofaa kwa ajili ya kilimo cha mizabibu

- Chagua eneo lisilokuwa na kivuli
- Eneo lenye udongo wa tifutifu usiotuamisha maji.
- Eneo liwe karibu na chanzo cha maji ya uhakika.
- Eneo ambalo meza ya maji (water table) ipo juu hupunguza gharama za umwagiliaji

### Maandalizi ya shamba

- Pima ukubwa wa shamba kabla ya kuanza maandalizi
- Fyeka nyasi, miti, chimbua visiki na mizizi kisha fukia mashimo yote na sawazisha shamba.
- Choma masalia ya mimea ili kuua fangasi aina ya *Armillaria mellea* ambaye husababisha kuoza kwa mizizi ya mizabibu.

### Njia za kuandaa shamba la mizabibu

Kuna njia kuu mbili za kuandaa shamba la mizabibu

#### 1. Mitaro

- Njia ya mitaro inafaa kwenye maeneo tambarare.
- Pima shamba kwa kutumia kamba na futi kamba kwa nafasi ya mita 2.5 mstari hadi mstari kwa kufuata ulekeo wa Mashariki kwenda Magharibi.

- Kabla ya kuchimba mtaro pima sentimita 45 upande wa kulia wa kamba na sentimetra 45 upande wa kushoto wa kamba kwenye kila mstari ili kupata upana wa sentimetra 90.
- Chimba mtaro wenyewe kina cha sentimetra 90.
- Wakati wa kuchimba mitaro tenganisha udongo wa juu wa kina cha sentimita 60 na udongo wa chini wa kina cha sentimita 30.
- Wakati wa kufukia mitaro changanya mbolea na udongo wa juu kwa uwiano wa 1:2 kwa kuwa udongo wa juu ndio wenyewe rutuba.
- Njia ya mitaro ni nzuri zaidi ukilinganisha na njia ya mashimo
- Mitaro huwezesha mizizi ya mizabibu kutawanyika vizuri kwa kujipatia virutubisho vya kutosha.
- Mtaro mmoja wenyewe urefu wa mita 64 huhitaji tani 3.5 za mbolea ya samadi ambayo sawa na tani 87.5 kwa ekari moja.



Mtaro wa sentimita 90x90 upana na kina na urefu wa mita 64

#### 2. Mashimo

- Njia ya mshimo inafaa katika maeneo yenye mteremko mkali
- Baada ya kupima shamba na kuweka mambo, funga kamba kwa nafasi ya mita 2.5 mstari hadi mstari na mita 1.5 shimo na shimo
- Chimba mashimo yenye vipimo vya sentimita 90x90x90, upana urefu na kina
- Wakati wa kuchimba mashimo tenganisha udongo wa juu wa kina cha sentimita 60 na udongo wa chini wa kina cha sentimita 30.
- Changanya mbolea na udongo wa juu kwa uwiano wa 1:2 (mbolea : udongo)

#### Kuweka viegemezo

Mizabibu ni mimea inayotambaa hivyo ni muhimu kuweka viegemezo. Viegemezo vinaweza kuwa vya nguzo/miti (Wooden poles) au vya zege (concrete poles).

#### Faida za viegemezo

- Hurahisisha upuliziaji wa dawa, kupalilia, kukatia na uvunaji wa zabibu shambani
- Hukinga mimea dhidi ya magonjwa na wadudu waharibifu
- Huruhusu mwanga wa juu na mzunguko wa hewa kuingia shambani kwa urahisi

## Namna ya kuweka viegemezo

- Weka viegemezo shambani kipindi cha ukuaji wa mizabibu.
- Nguzo za pembeni ziwekwe nanga ya jiwe au chuma na ziwekwe kwa ulalo (slanting).
- Weka viegemezo kila baada ya mashina manne au matano
- Funga waya wa kwanza sentimita 80-90 toka ardhini unene wa waya ni milimita 10
- Funga waya wa pili sentimeta 50-60 toka waya wa kwanza.
- Funga waya wa tatu sentimita 45-50 toka waya wa pili.

## Ukuzaji wa Mizabibu

- Fungia mche wa mzabibu kwa kamba kila unapokua.
- Pogolea machipukizi kila yanapoota.

## Kurejesha rutuba kwenye shamba la mizabibu ya zamani

- Kawaida mbolea ya samadi iliyowekwa kwenye shamba la mizabibu hupungua uwezo wake wa kurutubisha udongo kadri inavyotumika.
- Hivyo ni muhimu kurejesha mbolea kwenye shamba kila baada ya miaka mitano hadi saba
- Wakati wa kurejesha mbolea chimba mtaro umbali wa sm 75-80 kutoka shina

la mzabibu, mtaro uwe na upana wa sm 30 na kina cha sm 60

- Baada ya kuchimba mtaro changanya mbolea na udongo kwa uwiano wa 1:2
- Inashauriwa kurudishia mbolea upande mmoja wa mstari mwaka wa kwanza na upande wa pili mwaka unaofuata ili kuepuka kuua mizizi ya mizabibu

## Upandaji wa Miche ya Mizabibu Shambani

- Chimba shimo ndani ya mtaro kina cha sm 30, mwagilia maji na nyunyizia kiuatilifu cha kuzuia mchwa kama Gamalin au Attakan 350
- Panda miche kwa nafasi ya mita 1.5 katika ya mche na mche.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**  
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI),  
Kituo cha Makutupora,  
S.L.P 1676,  
Dodoma, Tanzania  
Simu: +255 26 2961994,  
Barua pepe: cdmakutupora@tari.go.tz

## TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA



## MAANDALIZI YA SHAMBA LA MIZABIBU NA UPANDAJI

